

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2013
MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA KIBWEZI
KIDATO CHA NNE 2013
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

- (a) Jibu maswali manne pekee.
- (b) Swali la kwanza ni la lazima.
- (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki : yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi.
- (d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- (e) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.

1. SEHEMU YA A : USHAIRI

BALAA

Na uwe mtenda mema, kwa wanalifu kutenda,
Mali ya haki kichuma, ukilima na kupanda,
Yaweza kuja zahama, yabalaa kukuganda,
Japo baya kukutenda, balaa laweza kuja.

Balaa laweza kuja, na jiwe likakuponda,
Na fujo za kukufuja, ikakupitia inda,
Kujitunza siyo hoja, japokuwa wajilinda,
Japo baya kukutenda, balaa laweza kuja.

Na hata misikitini, fujo huja zikatanda,
Pia humo kanisani, wevi huja wakapanda,
Huiba madhabauni, na kusikata mikanda,
Japo baya kukutenda, balaa laweza kuja.

Lala usingizi sana, ukumbatie makinda,
Huna na mtu fitina, watu wote wawapenda,
Watakuja kukuchana, kama ndege na matunda,
Japo baya kukutenda, balaa laweza kuja.

Maswali

- (a) Eleza njia tano ambazo balaa inaweza kukuja. (alama 5)
- (b) Eleza maana ya mshororo wa mwisho “Japo baya kukutenda, balaa laweza kuja.” (alama 2)
- (c) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (d) Bainisha vipengele vifuatavyo katika shairi .
- (i) Taswira
- (ii) Tashibihi. (alama 4)
- (e) Eleza uhuru wa kishairi uliotumika katika ubeti wa nne. (alama 2)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumikakatika hairi.
- (i) Kichuma (alama 1)
- (ii) Mkainda (alama 1)
- (iii) Madhabauni. (alama 1)

SEHEMU YA B: TAMTHILIA

Timothy M. Arege

Jibu swali la 2 au la 3

2. Baraza la mji wa Cheneo limejaa kila aina ya shida. Kwa kuitolea kauli hii mifano jadili matatizo yoyote kumi. (alama 20)
3. “Mwandametu. Dawa tulizonazo ni pain killers tu ! Afadhali kufanya jambo kuliko kutofanya kabisa. Labda itauwezesha mshumaa kuwaka hadi meli zinazosubiriwa zimalize kupambana na mawimbi.”

KIBWEZI DISTRICT FORM 4 INTER – SCHOOLS EXAM KISWAHILI P.3 2

- (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Taja tamathali moja iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
- (c) Fafanua hali ya matibabu katika mji wa Cheneo. (alama 14)

HADITHI FUPI – SEHEMU C

Jibu swali la 4 au la 5.

4. DAMU NYEUSI na Ken Walibora.
Fafanua aina mbalimbali za ubaguzi unaojitokeza katika hadithi ya Damu Nyeusi. Tolea kauli hii mifano kutoka kwa kitabu. (alama 20)
- Au
5. Mke Wangu na Mohammed Said Abdulla
(a) Eleza nafsi ya msimulizi iliyotumika katika hadithi ya “MKE WANGU” (alama 2)
(b) Taja aina tatu za wasichana msimulizi alitaka kuchagua mchumba kisha upeane mifano. (alama 6)
(c) Taja udhaifu wa Aziza kama vile alivyokuja kuugundua msimulizi wa hadithi hii. (alama 12)

SEHEMU YA D : FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 6 au 7

6. Eleza sifa za vipengele vya Fasihi Simulizi vifuatavyo.
(i) Nahau (alama 10)
(ii) Ushirikina (alama 10)
7. (a) Eleza maana ya maapizo. (alama 2)
(b) Taja sifa zozote tano za maapizo. (alama 5)
(c) Maapizo yana umuhimu gani katika jamii. (alama 10)
(d) Taja maapizo matatu katika jamii za kisasa. (alama 3)

SEHEMU YA E : RIWAYA

Said A. Mohammed – Utengano

Jibu swali la 8a au 8b

8. (a) “ ... Wewe kwako toka lini mwanamke kuwa mtu ? Wangapi umewatenda?”
- (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (ii) Kwa kutoa mifano mine mwafaka, dhihirisha ukweli wa dondoo hili. (alama 16)
- Au
- (b) Kwa kurejelea vipengele vifuatavyo vya matumizi ya lugha katika riwaya ya Utengano onyesha jinsi mwandishi amevitumia kufanikisha maudhui.
- (i) Uzungumzi nafsia. (alama 10)
- (ii) Taswira. (alama 10)

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs